REF. PSLE 2026

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# RATIBA YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI (PRIMARY SCHOOL LEAVING EXAMINATION TIMETABLE) SEPTEMBA, 2026

| TAREHE NA SIKU | MUDA (SAA) | NAMBA MFICHO | SOMO |
|---|---|---|---|
| **09.09.2026 JUMATANO** | 2:00 – 3:40 | 01 | KISWAHILI |
| | **3:40 – 4:30** | | **MAPUMZIKO** |
| | 4:30 – 6:30 | 04<br>04E | HISABATI<br>MATHEMATICS |
| | **6:30 – 8:30** | | **MAPUMZIKO** |
| | 8:30 – 10:00 | 06<br>06E | URAIA NA MAADILI<br>CIVIC AND MORAL EDUCATION |
| | | | |
| **10.09.2026 ALHAMISI** | 2:00 – 3:40 | 02 | ENGLISH LANGUAGE |
| | **3:40 – 4:30** | | **MAPUMZIKO** |
| | 4:30 – 6:00 | 05<br>05E | SAYANSI NA TEKNOLOJIA<br>SCIENCE AND TECHNOLOGY |
| | **6:00 – 8:00** | | **MAPUMZIKO** |
| | 8:00 – 9:30 | 03<br>03E | MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI<br>SOCIAL STUDIES AND VOCATIONAL SKILLS |

# MAELEKEZO MUHIMU

1. Hakikisha kuwa unayo **Ratiba ya Mtihani ya mwaka 2026** iliyoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

2. Hakikisha kwamba **unasoma jina la somo juu ya bahasha husika** na kuthibitisha kuwa somo hilo ndilo linalostahili kufanyika wakati huo kulingana na **Ratiba ya Mtihani**.

3. Kabla ya kufungua bahasha, mpe Mtahiniwa asome **kwa sauti** jina la somo lililoandikwa juu ya bahasha ili kuthibitisha ni somo husika kwa mujibu wa ratiba.

4. Endapo utata utajitokeza kati ya **maelekezo yaliyomo katika Karatasi ya Mtihani** na **Ratiba ya Mtihani**, **maelekezo yaliyomo katika karatasi ya Mtihani husika ndiyo yatakayofuatwa**.

5. Watahiniwa wenye mahitaji Maalum (**Wasioona, Uoni hafifu, Viziwi**) waongezewe **MUDA WA ZIADA WA DAKIKA 20 KWA KILA SAA** kwa somo la **Hisabati** na **DAKIKA 10 KWA KILA SAA** kwa masomo mengine.

6. Watahiniwa wenye **UONI HAFIFU** wapewe karatasi za Mtihani zenye **maandishi yaliyokuzwa,** zilizoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania kwa matumizi yao.

7. Watahiniwa waelekezwe;

    (a) Kuingia ndani ya chumba cha Mtihani nusu saa kabla ya muda wa Mtihani na watakaochelewa kwa zaidi ya nusu saa baada ya Mtihani kuanza hawataruhusiwa.

    (b) Kufuata maelekezo yote yatakayotolewa na wasimamizi wa Mtihani.

    (c) Kuandika namba ya Mtihani kwa usahihi.

    (d) Kutofanya mawasiliano ya maneno au kwa njia yoyote baina yao. Ikiwa Mtahiniwa ana tatizo anatakiwa kunyoosha mkono ili kuomba msaada kwa msimamizi wa Mtihani.

    (e) Kutojihusisha na vitendo vya udanganyifu katika Mtihani kwani watakaojihusisha matokeo yao yatafutwa.